JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA **(TAMISEMI)**

SHULE YA SEKONDARI KATESH

S.L P.199

KATESH –HANANG,

19/11/2021

SIMU: +255 789934217/+255 788 696 266

BARUA PEPE: katehsekondary@gmail.com

KUMB.NA…….

JINA LA MWANFUNZI……..

SHULE YA MSINGI ATOKAYO……

SHULE ALIYOCHAGULIWA KUJIUNGA ……WILAYA ……MKOA ……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KATESH (JOINING INSTRUCTIONS 2021)

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Katesh, mwaka 2021.Shule ya Sekondari Katesh ipo umbali wa kilomita 4.0 Kusini mwa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Hanang'.

Kwa wanaotoka mbali usafiri wa bodaboda kutoka mjini hadi shuleni unapatikana kituo kikuu cha mabasi kwa (Tsh. 1000/=) Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 17/01/2022 na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 21/01/2022

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA ANAPPORIPOTI SHULENI

(a) Sare za Shule

Wavulana

- Sare za shule hii kwa wavulana ni suruali (2) zenye rangi za dark blue zenye mshono wa rinda ,celebration yenye mkunjo wa chini /turn up.
- Shati nyeupe yenye mikono mifupi isiyobana (pea 2)
- Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi vya kamba (Pea 2)
- Soksi yenye rangi ya Khaki (pea zaidi ya moja)
- Sweta mbili zenye rangi ya dark blue (pea 2)
- Sare za michezo (bukta 01 yenye rangi ya bluu na fulana 01 yenye rangi ya njano na viatu vya raba yoyote.

Wasichana:

- Sare za shule hii kwa wasichana ni sketi (2) zenye rangi za dark blue zenye rinda box,ndefu mpaka chini ya heshima.

- Shati rangi nyeupe yenye mikono mifupi isiyobana (pea 2)
- Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi vya kamba (Pea 2)
- Soksi yenye rangi nyeupe (pea zaidi ya moja)
- Sweta mbili zenye rangi ya dark blue (pea 2)
- Kwa wanafunzi wa dhehebu ya **KIISLAMU,washone HIJAB** rangi nyeupe ,short Kanzu yenye rangi nyeupe ya mikono mirefu isiyobana,na suruali ya rangi ya dark bluu (pea 2)
- Sare za michezo (bukta 01 yenye rangi ya bluu na fulana 01 yenye rangi ya njano na viatu vya raba yoyote.

  NB. KITAMBAA GRADE 1 (ONE)

3.0 VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI

- Madaftari kumi na moja (11) aina ya Counter books Quire 2, MathematicaL SET 01, rula 01, Kalamu na penseli za kutosha.
- Vyombo vya kulia chakula (sahani,kijiko,na bakuli (Aluminium)
- Chakula cha wanafunzi wa kutwa utaratibu wake utasimamiwa na kamati ya chakula ya wazazi ambapo kila mwanafunzi atachangia kiasi cha Tzs.120, 000/= kwa mwaka kupitia akaunti ya wazazi namba NMB **41010006284** (WAZAZI KATESH SEKONDARI) -Kila mwanafunzi atawasilisha Bank pay in Slip kwa kamati ya chakula siku atakaporipoti shuleni, vinginevyo hatapokelewa.
- Matibabu ya mwanafunzi yatagharimikiwa na wazazi wenyewe.
- Kila mwanafunzi aje na bunda moja ya karatasi ‘REAM’ kwa ajili ya mazoezi ya masomo mbalimbali ya ndani

KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI KATESH

_____

BHAHANDI NTAHONDI BHEDETSE

K/MKUU WA SHULE

3:0: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha unazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais- Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maa ndishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi asubuhi na mapema kila siku katika siku za masomo ni jambo la lazima.
e) Kushiriki shughuli za shule na nyingine utakazopewa ni lazima
f) Kufahamu mipaka ya shule kwa kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka wakati wote wa uwanafunzi wako ndani ya shule hii.
g) Kutunza usafi wa shule , mwili, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla ni lazima.
h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa(suruali inayokubalika ambayo siyo minyonyo na sketi ndefu ya heshima kwa wasichana iwe chini ya magoti)
i) Kuwa na nywele fupi inayotakiwaa na siyo ndefu au kuwa na panki au kiduku wakati wote uwapo shule.
j) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
k) Kutunza mali za umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi.
b) Uasherati na Ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
e) Kupiga au kupigana
f) Kutovaa kwa heshima mfano (kuvaa suruali chini ya makalio (milegezo) kutochomekea shati au fulana
g) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
h) Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
i) Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito.

j) Kuoa au kuolewa.

k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

l) Kukataa adhabu kwa makusudi .

m) Kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu kama vile laini, chaja, memori kadi n.k

4:0: MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical examination form, ambayo inajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali . fomu hii itakabidhiwa ofisi ya Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni .

b) Fomu ya maelezo binafsi na mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5:0. Tafadhali soma kwa makini maelezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA **(TAMISEMI)**

SHULE YA SEKONDARI KATESH

S.L P.199

KATESH –HANANG,

19/11/2021

SIMU: +255 789934217/+255 788 696 266

BARUA PEPE: katehsekondary@gmail.com

KUMB.NA…….

FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA / WILAYA AU HOSPITALI NYINGINE ZINAZOTAMBULIWA NA SERIKALI, NA MWANAFUNZI AJE NA HII FOMU PINDI ANAPORIPOTI.

Mimi / Jina la Mganga …….

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la Mwanafunzi…… Amepima kikamilifu na kuonekana kuwa ana/hana afya nzuri kwa mujibu wa Taarifa zifuatazo”

A: HALI YA MWILI

1. Mapigo ya moyo ……..
2. Haemoglobin HB ……..
3. Kundi la damu ……..
4. Mkojo (Urine) ……
5. Kinyesi (Stool) ……
6. Macho (yana kasoro) Eye test ……
7. Masikio (yana kasoro) ……
8. Pumu (Arthma)…….
9. Kifua kikuu (TB) ……
10. Kifafa (Epilepsy) ……
11. Shinikizo la damu la juu/chini (Blood Pressure) ……
12. Vidonda vya tumbo (Ulcers) ……
13. Maradhi ya zinaa ……
14. Ukoma (Leprosy) ……
15. Ugonjwa wa akili (mental illness) ……

16. Maradhi mengineyo makali ambayo hayajatajwa hapo juu kama yapo ……

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA **(TAMISEMI)**
SHULE YA SEKONDARI KATESH

S.L P.199
KATESH –HANANG,

19/11/2021

SIMU: +255 789934217/+255 788 696 266
BARUA PEPE: katehsekondary@gmail.com
KUMB.NA…….

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO MAKOSA YA JINAI.

(FOMU YA MAPOKEZI SHULENI)
SEHEMU A: IJAZWE NA MWANAFUNZI

Mimi …….. nakubali kutii sheria zote za shule kama zilivyoainishwa hapo juu, sitashiriki katika migomo yoyote ile, fujo na makosa mengine ya jinai.

Saini ya mwanafunzi …….. Tarehe ……..

SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

1. Jina la mzazi/mlezi…….
2. Anwani ya mzazi/mlezi ……
3. Namba ya simu ya mzazi/mlezi 1.……2……..
4. Mahali a napoishi (kijiji) kata …….
5. Kazi ya mzazi/mlezi ……
6. Mahali anapofanyia kazi …….

SEHEMU C: IJAZWE NA MZAZI/MEZI

Mimi ……. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……. Ninakiri kukubaliana na sheria. kanuni na maelekezo yote mengine yatakayotolewa na shule. Pamoja na hayo nipo/sipo tayari kushirikiana na walimu wakati wowote nitakapohitajika kutoa ushirikiano wangu.

Saini ya mzazi/mlezi …… Tarehe ……